



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb: Na. CHAL/L. D/4088

30.11.2025

**MKURUGENZI MTENDAJI,
TISEZA,
S. L.P. 938,
DAE ES SALAAM.**

**YAH: UTHIBITISHO WA UMILIKI WA KIWANJA NAMBA 6 KITALU 18B TONGA
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE.**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

2. Awali eneo hili la Ardhi lilikuwa linamilikiwa kienyeji kama shamba na wananchi wazawa wapatao 3 ambao waliuza mashamba yao kwa Ndugu Mathias Adolph Kingalu mwaka 2008 yenye ukubwa wa ekari 3.45, ambapo ndugu Mathias Adolph Kingalu aliwauzia Kampuni ya **HUSSAIN GRINDING MILLS LIMITED** ya S.L.P 1050, Dar es salaam.

3. Kampuni hiyo ililipa stahili za mwananchi huyo kwa kuzingatia makubaliano yaliyowekwa kati ya wananchi na kampuni tajwa na baadaye kuwasilisha ombi la umilikishaji kwenye Halmashauri ya kijiji cha Tonga.

4. Baada ya kampuni kukamilisha taratibu za kulipa stahili za wamiliki asili, maombi ya kumiliki ardhi hiyo yalijadiliwa na Halmashauri ya kijiji cha Tonga tarehe **08.04.2024** na mapendekezo ya kikao cha Halmaushari ya kijiji yaliwasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji cha Tonga uliofanyika tarehe **25.14.2024** ambapo kwa mujibu wa **Sheria ya Ardhi ya kijiji sura ya 114**, kijiji kilipendekeza mwombaji apewe eneo hilo lenye ukubwa wa ekari 3.4 (Muhtasari wa Halmashauri ya Kijiji, Mkutano Mkuu wa kijiji na mikataba ya mauziano imeambatanishwa kwa marejeo yako).

5. Baadaye ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Chalinze ilipokea barua ya tarehe 16/12/2024 ya kuomba kupimiwa ardhi hiyo. Wataalam walitembelea eneo hilo na kubaini halina mgogoro wowote na baadaye ulibuniwa mchoro wa Mipango Miji Nambari TP. DRG. NO.19/CDC/623/012025 ulioidhinishwa na Mkurugenzi wa Mipangomiji na Vijiji Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa matumizi ya **Viwanda (Use Group "N" Industry Use classes (a) and (b) as defined in UPA No. 8 of 2007.**"
6. Aidha upimaji wa ardhi hiyo ulifanyika na ramani kupata kibali cha Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliyosajiliwa kwa namba **PWNSP00001198** na kupatikana kiwanja namba **6 kitalu "18B" TONGA.**
7. Kwa kuwa kampuni inayoomba ardhi ni ya kigeni; Kampuni ya **"HUSSAIN GRINDING MILLS LIMITED"** imewasilisha:
- Mikataba ya mauziano ya Wananchi wazawa wapatao 3,
 - Muhtasari wa Halmashauri ya Kijiji na Mkutano mkuu wa Kijiji
 - Udhibitisho wa uraia /pasi za kusafiria za Wakurugenzi,
 - Certificate of incorporation of a Company,
 - Certificate of registration,
 - TIN number,
 - Business License,
 - Tax clearance certificate
 - Ramani ya upimaji wa kiwanja Na 6 kitalu 18B
8. Kwa barua hii, nathibitisha kuwa kiwanja Namba **6 Kitalu 18B Tonga** hakina mgogoro wowote nawasilisha kwako kwa hatua zaidi.
9. Natanguliza shukrani.

Ramadhan S. Possi
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
CHALINZE

